
wanyamapori tanzania

# Kakakuona



# Januari Mosi Kila Mwaka Ni Siku ya Taifa ya Kupanda Miti



Tarehe 1 Januari mwaka 2000 Rais Benjamin Mkapa alizindua kampeni ya "Otesha Mti wa Milenia Mpya". Madhumuni ya kampeni hii ilikuwa ni kuweka kumbukumbu ya ujio wa Milenia ya Tatu na kuwahamasisha wananchi kupanda miti ili kuhifadhi mazingira katika kurejesha miti ambayo ni muhimu sana katika kuhifadhi mazingira na kukidhi mahitaji ya wananchi.

Wakati wa Uzinduzi, Rais Mkapa alitoa rai kuwa Watanzania tujenge utamaduni wa kupanda miti. Aidha, Wizara ya Maliasili na Utalii ilishauri na Mheshimiwa Rais alikubali kimsingi kwamba kila siku ya kwanza ya mwaka katika Milenia ya Tatu,Watanzania pamoja na mambo mengine, washerehekee kwa kupanda miti.

**Rais amekubali rasmi kwamba tarehe Mosi Januari isherehekewe kwa kupanda miti. Wananchi pote nchini wanatakiwa kuisherehekea siku hiyo kwa kupanda miti.**

Ili kuhakikisha kuwa wananchi wanatekeleza wajibu wao wa kupanda miti tarehe Mosi Januari kila mwaka, Wizara ya Maliasili na Utalii inakusudia kushirikisha Wizara zenye uhusiano na masuala ya mazingira,taasisi mbalimbali za hapa nchini na za kimataifa pamoja na viongozi wa Mikoa na Wilaya katika kuandaa programu za utekelezaji.

Halmashauri za Wilaya, ambazo ziko karibu zaidi na wananchi, zinaaswa kuwa mstari wa mbele. Vyombo vya habari vitashirikishwa kikamilifu ili vieweze kufikisha ujumbe wa Siku ya Taifa ya Kupanda Miti. Mkazo utiliwe katika upandaji wa miti ya asili. Mradi wa Mbegu za miti una mbegu za kutosha za miti ya asili katika vituo vyake vya Morogoro,Lushoto na Iringa.

Kwa kushirikisha wananchi katika kuotesha miti kila Januari Mosi tutaweza kujenga utamaduni wa kupanda miti ambao utakuwa wa manufaa kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Aidha, taifa litapata mafanikio makubwa.


**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII.**

wanyamapori tanzania

# Kakakuona

Linatolewa pamoja na gazeti la

**wildlife**



## Ofisi ya Mhariri:

Ivory Room,
Makutano ya Barabara ya Nyerere,Barabara ya Chang'ombe na Barabara Mpya ya Kawawa
S.L.P 1994 Dar es Salaam.
Simu: 2866377, 0784 402927-8
Fax: 2865500.
Waraka umeme (Email):kakakuona@africaonline.co.tz
Tovuti:http//www.newafrica.com/tanzaniawildlife

**Mhariri Mkuu:** John Waluye

**Mhariri Msaidizi:** Tabu Ndziku



**Usanifu na Uchapaji:** Tanzania Printers Limited, Dar es Salaam.


## Maulizo kuhusu mauzo na matangazo ya Biashara:

**Dar es Salaam:**
Ofisi ya Mhariri, S.L.P 1994, Dar es Salaam

**Usambazaji:**
Kakakuona linapatikana katika maduka yote makubwa ya vitabu, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam, Mahoteli makubwa, Ofisi za Wanyamapori na Maliasili Mikoani.

**Wauzaji wakuu:**
**Dar es Salaam:**
Duka la vitabu la Tanzania Publishing House,
Mtaa wa Samora,
Lango kuu la Ivory - Room,

**Arusha:**
KASE Bookshop
Kilimahama Literature Centre
Malihai Clubs of Tanzania

**Zanzibar:**
Masomo Bookshop

**Mwanza:**
Malihai Clubs of Tanzania Pasiansi

**Moshi:**
Crane Craft Shop
Chuo cha Wanyamapori -College of African Wildlife Management,Mweka

**Morogoro:**
Duka la Vitabu la Chuo Kikuu Cha Sokoine

**Dodoma:**
Dodoma Environmental Network (DONET)
Pori la Akiba Swagaswaga

**Mbeya:**
Pori la Akiba Usangu


14/12/2020
LIBRARY



**KAKAKUONA** linachapishwa mara nne kwa mwaka na Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - *Tanzania Wildlife Protection Fund* (TWPF), chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.


**Kwa maelezo zaidi kuhusu TWPF, wasiliana na:**


Katibu Tawala

S.L.P. 1994, Dar es Salaam

Simu: 2866377, 0784 402982
Fax: 2863496.
Waraka umeme (Email): kakakuona@africaonline.co.tz




## Bodi ya Wadhamini wa TWPF:

Prof. Salome Misana (Mwenyekiti)
Mhe. Lekule Laizer (Mb), Bw. Eliachim Simpasa
Bw. E.B Chausi, Bw. Gerald Bigurube,
Bw. Emmanuel Severre.
**Katibu Tawala:** Bw.Paul I. Sarakikya
**Afisa Miradi:** Bw. Alfonce Ambrose Mung'ong'o
**Mhasibu Mkuu:** Bw. Lawrence M. Munale


# YALIYOMO

Picha ya Jalada: Nungunungu






Matukio ya wanyamapori niliyoyaona zamani..............................5



Jangili akatwa mguu na Mamba ..................................................10



Hongera NALIKA kwa Uhifadhi wa Wanyamapori .......................22

Tahariri

# Tuache Uharibifu wa mazingira




Taarifa za wataalam zinaonyesha kuwa vina vya maji katika Ziwa Victiria na Ziwa Rukwa vimepungua sana kutokana na uharibifu wa mazingira ambao nchi zilizoendelea hupendelea kuuita ' Mabadiliko ya Hali ya Hewa" ili kuficha ukweli wakati ni matokeo ya uharibifu wa mazinbgira.

Kwa ujumla , mabadiliko ya hali ya hewa ni matokeo ya uharibifu wa mazingira unaotokana na binadamu, pia hutokana na kazi za viwandani ambazo pia zimekuwa zikisababisha moshi ambao huharibu kiambaza kinachozuia watu wasiathirike na miale ya jua.

Wataalam wamebainisha kuwa uharibifu huu wa kiambaza kinachozuia miale ya jua kinaacha matundu ambayo yanapitisha miale hatari ya jua na kusababisha madhara mbalimbaliu kwa wanadamu. Baadhi ya matatizo yaliyoonekana kutokana na tatizo hili ni kansa ya ngozi, ongezeko la joto duniani ambalo linasababisha myeyuko wa barafu kutoka mwambao wa Kusini na Kaskazini, Kuyeyuka kwa thelui juu ya kilele cha Mlima. Kilimanjaro na vivyo hivyo kuleta mafuriko, vimbunga, ukame pamoja na joto kali.

Uharibifu wa misitu kwa kukata miti kwa ajili ya kuni, mkaa, mbao pamoja na kukata miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo kama ujenzi wa barabara kubwa au mashamba makubwa inasababisha uharibifu wa mazingira. Ukataji wa miti unasababisha gesi aina ya 'carbondioxide' kuongezeka kwa joto duniani. Miti husaidia sana kuipooza dunia pamoja na kufyonza gesi zote ambazo ni sumu, kutengeneza mvua, kuufunika uso wa dunia na kuzuia mmomonyoko wa udongo.

Ripoti ya hivi karibuni kutoka Chama cha Kitaifa cha Wataalam wa Mazingira nchini Uganda (Uganda National Association of Proffessional Environmentalists - NAPE) inaonyesha kushuka kwa kina cha maji cha Ziwa Victoria kwa mita mbili jambo ambalo linahitaji kuangaliwa kwa umakini kwa sababu ni hatari.

Ripoti hiyo inaoonyesha kuwa kupungua kwa kasi kwa maji katika Ziwa hilo ni kujengwa kwa Bwawa la Kiira kandokando ya Bwawa la Nakubaale pembezoni mwa Mto Nile, nchini Uganda ambalo linasababisha maji kutoka katika ziwa na kuelekea huko.

Tatizo hilo si la Uganda tu bali linawaathiri watu wa nchi zote wanaopata huduma kutoka ziwa hilo ikiwemo Tanzania ambayo meli zinazopita ziwani humo ziko hatarini kutokana na kushuka kwa kina cha maji.

Mpango wa Usimamizi wa kulitunza Ziwa hilo ulianzishwa mwaka 1997 ambapo wajumbe wa kamati hiyo walitoka katika nchi za Kenya, Uganda na Tanzania ili kulitunza ziwa hilo kwa faida ya nchi zote tatu, lakini inaonekana mpango huo haufanyi kazi ipasavyo. Kila nchi mwanachama inaonekana hutumia ziwa hilo apendavyo bila kuwahusisha wanachama wenzake.

Kukosekana kwa mvua katika eneo la kukusanyia maji la mto Kagera unaopeleka maji katika Ziwa Victoria pia ni moja ya sababu ya kushuka kwa kasi kwa kina cha maji katika Ziwa hilo. Si hivyo tu bali pia ongezeka la matumizi ya maji kutoka ziwa hili kumeongezeka kwa kasi kutokana na idadi ya watu ambao wanaishi pembezoni mwa ziwa hilo.

Upungufu wa maji katika Ziwa Victoria ambalo ni la pili kwa ukubwa duniani, linahatarisha maisha ya viumbe vingine vinavyoishi katika ziwa hilo kama vile samaki, wanyama, ndege, pamoja na viumbe vingine vinavyoishi kandokando ya ziwa.

Vilevile mamba ambao huishi katika Ziwa Rukwa mkoani Rukwa pamoja na viumbe waiishio katika Ziwa Jipe lililoko Wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro mpakani mwa Kenya na Tanzania wako hatarini kutokana na maziwa hayo kuanza kukauka. Hii imetokana na mwanadamu kuharibu mazingira kwa kukata misitu iliyo kando kando ya maziwa hayo.


Kwa upande wa ziwa Rukwa, kwa mfano, kukauka kwa ziwa hilo kunatokana na walimaji wa tumbako wa mkoa huo kukata miti ovyo ili kupata kuni kwa ajili ya kukaushia tumbaku pamoja na ukataji wa miti ambayo hutumika kutengenezea vitalu vya kuoteshea mbegu kwa ajili ya zao hili. Ukataji huo wa miti unaleta upungufu wa mvua na pia kupunguza kina cha maji ya mito na vijito.

Tatizo la maji ni kubwa na si kwa Tanzania tu, bali ni kwa ulimwengu mzima. Kuna kila sababu ya watu kutunza misitu na pia kutunza vyanzo vya maji na kutokukata miiti ovyo ili kuondoa tatizo hili ulimwenguni kote.

Kutokana na kuwa uharibifu wa mazingira unatokana na shughuli za kila siku za mwanadamu, lakini wakati umefika kwa kwa serikali na raia kushirikiana ili kuondoa tatizo hili na kuokoa maisha ya wanadamu na viumbe vingine pamoja na kutunza mazingira yetu.

# Matukio ya Wanyamapori niliyoyaona zamani

Na Charles M. Njali




Charles Njali (kulia) akiwa ameegemea basi aina ya Albion alimokuwa anafanyia kazi miaka ya 1960 akiwa pamoja na dereva wake Ezekiah (kushoto) na utingo Mzee Paulo aliyekaa chini

**MWAKA** 1957 wakati nafanya kazi Idara ya Reli na Bandari ya Afrika Mashariki kama kondakta wa basi sehemu ya kusafirisha abiria kutoka Iringa mpaka Dar es Salaam, kuna mkasa uliotokea ambao naona si vibaya kuwasimulia ingawaje imepita takribani miaka 50 hivi.

Mimi nikiwa kama kondakta wa basi, tuliondoka Iringa saa mbilikamili asubuhi na kufika Mikumi saa saba mchana. Msishangae kwanini tulitumia muda mrefu kusafiri kipande hicho wakati umbali kutoka Iringa hadi Mikumi siyo mrefu sana. Enzi hizo barabara ilikuwa ya udongo na sio lami kama ilivyo hivi sasa.

Tuliondoka Mikumi kuelekea Morogoro saa 7:15 na robo. Tulitembea maili 12 kutoka Mikumi tukiwa porini hamna hata nyumba. Hata hivyo nilishangaa baada ya kuona dereva amesimamisha gari ghafla kutokana na wadhifa wangu nililazimika kuteremka kuangalia kulikoni! Mimi na abiria takribani 20 hivi tulikuwa tumekaa chumba cha Daraja la Tatu.

Kwa ufahamisho tu, mabasi ya Shirika la Reli na Bandari enzi hizo yalikuwa na sehemu mbili – Daraja la Tatu na Daraja la Pili na Dereva alikuwa amekaa pekee yake ili asije akaleta ajali wakati anazungumza na abiria.

Abiria sita waliteremka kutoka kwenye basi na tukawa nje ya basi, abiria saba hivi kwa jumla tukawa tunaangalia kule mbele ya gari letu kuna nini? Ndipo tulimwona Tembo mmoja mkubwa amesimama katikati ya barabara umbali wa hatua thelathini hivi. Yule Tembo akaanza kuyachezesha masikio yake mapana na kuanza kuja upande tulikosimamia.

Mimi na abiria sita tulianza kukimbia ndani ya gari. Mlango wa basi ulikuwa ni mdogo kwani kila mmoja alitaka awe wa kwanza kuingia ndani. Dereva alipomwona yule Tembo akiwa amefika umbali wa hatua 15 hivi, akaiweka gea yake ya kurudi nyuma na basi likawa linarudi kinyume nyume.

Dereva alipoona Tembo amekaribia kama hatua saba hivi, alichanganyikiwa na kuanza kurudi nyuma bila kuangalia nyuma kuna nini kwa vile macho yetu wote yalikuwa kwenye Tembo. Kwa bahati mbaya basi letu likaligonga lile gari la mizigo. Taa moja ya upande wa kushoto ilivunjika.

Sisi tuligombania tu mlango wa bus ili tuingie ndani tukawahi kuingia. Abiria mmoja aliuliza: "Haya jamani, nani ana sigara na kiberiti?" ili avute sigara na moshi wa sigara apulizie upande wa Tembo alikosimama.





Mmoja wa abiria akafanya hivyo wakati huo Tembo akiwa yuko hatua tano akitazamana macho kwa macho na Dereva. Harufu ya sigara na kiberiti ilipomkuta Tembo, akigeuza njia, akaiacha barabara na kuelekea porini.

Wataalamu wa mambo ya porini wanasema Tembo atembeaye peke yake huwa ni mkali na mkorofi maneno hayo yalidhihirishwa na yule Tembo ambaye alionekana kuwa na shari. Mara kwa mara tembo hutembea katika makundi.

Baada ya yule Tembo kuelekea porini, tuliendelea na safari yetu mpaka Morogoro Polisi kwenda kuandikisha maelezo ya ile ajali ya basi letu kuligonga lori wakati tunamkimbia Tembo.


Tulivyomaliza ushahidi tuliruhusiwa na tukaanza tena kuendelea na safari yetu kuelekea Dar es Salaam, Railways Station.

Mwaka uliofuatia 1958 tena, nilikuwa natoka Mbeya kwenda Iringa na Gari la Abiria. Tulipofika Igawa, kilomita 136 hivi kutoka Mbeya, tulisimama ili tupate chakula cha mchana.

Baada ya kumaliza kula, tuliendelea tena safari yetu kuelekea Iringa tukiwa tumeshiba vema. Lakini tulipotoka Igawa tukiwa tumesafiri mwendo karibia maili saba hivi, dreva alisimamisha basi ghafla na kuanza kuniita kwa sauti: "Halo, je umewaona hao Chui? Kabla sijafungua mlango nilichungulia dirishani lakini sikuona kitu, ndipo nikafungua mlango wa gari.

Niliteremka chini na abiria watano tukawa watu sita chini. Sisi tulikuwa tumekaa katika chumba cha Daraja la Tatu. Tuliposhuka chini tulichungulia nyuma ya gari upande wa ng'ambo ya barabara tukamwona Chui mmoja

akiangalia gari letu kwa shingo upande



huku dereva akiliungurumisha gari kwa sauti ya resi mara kwa mara ili kuwastua wale Chui kwa mlio wa basi.

Kumbe jirani na pale tulipossimama alikuwepo Chui mwingine ambaye tulikuwa hatukumwona. Mara ghafla akaamua kutoka alipokuwa mgongoni kwetu na kukatiza kwenda kwa mwenzie upande wa pili wa barabara.

Wakati Chui akitupita ghafla, ule mlango wa basi ukaonekana mdogo maana kila mmoja alitaka awe wa kwanza kuingia. Tukasukumana na wanne waliwahi kuingia ndani ya basi. Nje tulibaki wawili, ila mwenzangu, akawa amepata mshtuko akashindwa hata kupanda ndani ya basi, akawa amelala pale chini ya mlango.

Nikamwambia ainuke lakini akawa ananitazama tu. Mshtuko wa yule chui alipopita karibu yetu ulimfadhaisha sana, mikono na miguu yake ikapata ganzi. Kuonana uso kwa uso na mnyama kama Chui au simba ni kazi kweli, heri usimuliwe tu.

Wale Chui wakakutana wakawa wawili wanatuangalia kama paka waangaliavyo. Nilimwomba abiria mmoja ateremke haraka aje tusaidiane ili tumwingize ndani ya basi yule abiria aliyekuwa hajiwezi. Bahati nzuri abiria mmoja akajitolea akateremka na tukamwingiza yule abiria ndani ya basi.

Wakati wote huo, yule abiria alikuwa hazungumzi. Kila tukimwuliza alikuwa kimya tu hadi tulipokwenda maili tatu hivi ndipo alianza kuzungumza kwa mbali kama mlevi.

"Tuna bahati sana leo hii. Chui ni wabaya sana. Migongo yao utafikiri wana mabawa. Chui ni wepesi sana na kwa muda mfupi anaweza akashambulia watu wengi. Mimi nilikuwa nasikia tu Chui Chui," alisema yule abiria.

Kwa kweli siku ile ilikuwa ni ya bahati yetu maana nasikia Chui ni hatari sana. Kweli Chui anaweza akawaparura na kuwajeruhi watu wengi kwa muda mfupi tu. Mara nyingi Chui hupenda kushambulia sehemu za usoni na kuvuta ngozi ya pua ambayo hufunika macho na hivyo kukushambulia atakavyo kwani utakuwa huoni.Baada ya mkasa huo, basi letu liliendelea na safari yake kuelekea Iringa.

Mkasa mwingine ulinitokea wakati nikisafiri kutoka Iringa kwenda Dodoma kupitia njia inayopita John's Corner, lakini wakati huu sikuwa nafanya kazi ya ukondakta bali nilikuwa abiria tu.

Tulipofika Bwawa la Mtera, basi letu lilisimama. Kama ilivyo kawaida ya watu wakifika mahali ambapo hawajawahi kufika huwa macho myamya. Kweli, tulipochungulia chini kule kwenye bwawa, tuliona sinema ya bure.

Tulimwona Mama Tembo na mtoto wake wakiogelea kutoka ng'ambo - Mama Tembo akiwa mbele na mtoto wake akifuata kwa nyuma. Kumbe wakiwa humo ndani ya maji, tulikuwa hatujui mambo yanavyoendelea.

Huku Mama Tembo akiogelea na mwanae, kumbe Mamba walikuwa wanamzamishazamisha yule mtoto wa Tembo mpaka wakafika ng'ambo ya pale nchi kavu. Mtoto wa Tembo, bahati nzuri naye akawa amevuka nchi kavu.


Alipotoka yule mtoto wa Tembo, kwa nyuma yake walifuata Mamba wanne ambao walikuwa ndani ya maji wakijaribu kumzamisha mtoto wa Tembo ili wamle. Kila mmoja wa wale Mamba alionekana kumtamani yule mtoto wa Tembo na ndiyo maana wakawa wajasiri kumfuata hata mama yake akiwepo.

Yule mtoto wa Tembo kumbe alikuwa amekunywa maji mengi hivyo alivyotoka tu ndani ya maji hakutembea hatua nyingi alianguka chini mbele ya mama yake. Mama Tembo akashangaa kulikoni na mtoto wake.

Mara Mama Tembo akawaona wale Mamba. Akawaendea wale Mamba na tukaona amemshika mmoja kwa mkonga wake na kumzunguusha akiwa juu na kumtupa mbali. Akamshika wa pili, watatu na wanne akawatupilia mbali kwa hasira ya kutaka kumuulia mwanae.

Bahati mbaya enzi hizo kulikuwa hakuna video kamera, hivyo tukio hili halikunaswa kwenye mkanda. Lakini kwa maelezo haya nadhani umefurahi kupata mkanda wa maneno toka kinywani mwangu.

Basi letu liliondoka pale Bwawa la Mtera kuelekea Dodoma na kila abiria akiwa amefurahia tukio hilo na safari nzima ilikuwa gumzo la wale Tembo na Mamba.



# Jangili akatwa
# akivua samaki Ihefu

Na John Makunga

**PAMOJA** na idadi kubwa ya wavuvi haramu kukamatwa na kutozwa faini kabla na wakati wa kipindi cha Operesheni ya Ihefu, bado wavuvi wameendelea kujipenyeza na kufanya uharibifu na uchafuzi wa mazingira katika eneo la ardhi-oevu ya Ihefu linalolindwa kwa mujibu wa sheria ya kuhifadhi wanyamapori ambayo haitoi nafasi ya shughuli za uvuvi katika mapori ya akiba.

Hivi karibuni kumeripotiwa kuwepo kwa tukio la mwananchi mmoja aliyetajwa kwa jina la Erick Sanga, mkazi wa kijiji cha Lupila, Wilaya ya Makete, Mkoani Iringa aliyenusurika kifo baada ya kuvamiwa na kukamatwa na mamba mwenye njaa.

Habari zimesema kwamba tukio hilo lilitokea katika eneo la Kidumka ambalo ni moja kati ya maeneo yaliyo na idadi kubwa ya mamba katika ardhi-oevu ya Ihefu.

Akieleza kuhusiana na tukio hilo, mkazi mmoja wa kijiji cha Ikoga kwa masharti ya kutoandikwa jina lake gazetini, alisema kwamba siku ya tukio mwananchi huyo akiwa ameambatana na mwenzake walioondoka asubuhi kutoka katika kambi yao ya uvuvi kwenda kukagua nyavu zilizokuwa zimetegwa jana yake. Wakati wakiendelea kufanya ukaguzi huo, ndipo ghafla alitokea mamba ambaye alikuwa akivizia mawindo yake nje ya mto. Wakati wavuvi wakiendelea na zoezi lao, ndipo mamba alipoweza kuukamata mguu wa mwananchi huyo kwa lengo la kujipatia kitoweo.

Kitendo hicho kilimfanya mvuvi Sanga kupiga kelele za kuomba msaada huku akiwa amefanikiwa kushikilia mti uliokuwa karibu naye na katika harakati za vuta nikuvute, mamba aliweza kuukata mguu wa mvuvi na kuondoka nao na kumwacha majeruhi akitokwa na damu nyingi.

Taarifa zimefahamisha kwamba, baada ya wavuvi wenzake kufika katika eneo la tukio walimchukua mwenzao na kumkimbiza katika Hospitali ya Misheni ya Ilembula iliyopo Wilayani Njombe, Mkoani Iringa kwa matibabu. Wenzake walimpeleka hospitali hiyo iliyoko mbali kulinganisha na hospitali ya Wilaya ya Mbalali, Mkoa wa Mbeya ili kujaribu kuficha taarifa kuhusiana na tukio hilo zisiwafikie askari wa vituo vya operesheni kwa hofu ya kutiwa nguvuni kwa kosa la kuingia na kufanya shughuli zao hifadhini kinyume cha sheria.

Polisi Wilayani Mbarali wamesema kuwa hakuna taarifa yoyote iliyopokelewa kuhusiana na tukio hilo na kuongeza kusema kuwa huenda wavuvi hao hawakuweza kuripoti katika kituo cha polisi baada ya tukio hilo kuogopa mkono wa sheria.

Hata hivyo jitihada za kumtafuta Mganga Mkuu wa Hospitali ya Misheni Ilembula kuthibitisha tukio hilo haziweza kufanikiwa. Habari kwa mujibu wa wasamaria wema zimedai kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja hivi, Sanga alikuwa akiishi katika kijiji cha Ikoga, Wilayani Mbarali kazi yake kubwa ikiwa ni uvuvi haramu katika eneo la Ihefu.

Ingawa serikali katika jitihada zake za kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji imekuwa ikitumia mbinu mahsusi ikiwemo elimu ya mazingira kwa jamii, wananchi wamekuwa wakiziba masikio na kuendeleza uharibifu ambao athari zake zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku. Matokeo yake usalama wa bioanuai zinazohifadhiwa umeendelea kuwa hatarini.



Licha ya hilo, wananchi wenyewe ambao ndio watumiaji wakubwa wa rasilimali hizo wamekuwa wakiathiriwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa vile jamii hiyo ya wavuvi mara nyingi imekuwa ikitumia dawa za kuulia

# nguu na mamba

wadudu waharibifu wa mazao katika shughuli zao za uvuvi haramu na hivyo kusababisha maangamizi makubwa kwa viumbe bila kubagua.

Aidha, wavuvi wenyewe wamekuwa wakijikuta katika mazingira magumu na ya hatari kwani vifo vyao vimekuwa vikisababishwa na ukosefu wa huduma za afya katika kambi zao na pia kutokana na uchafuzi wa mazingira ndani na nje ya maji. Kutokuwepo kwa vyoo katika kambi za wavuvi huchangia kwa kiasi kikubwa kusababisha magonjwa ya mlipuko kama vile kuhara, kuhara damu na kipindupindu hasa wakati wa majira ya mvua.


Tatizo jingine linalosababisha hali ya wasiwasi kwa maisha ya wavuvi ni kuwepo kwa wanyamapori wa hatari ambao aidha huwashambulia kwa nia ya kujihami wakiamini kuwa binadamu ndiye adui yao mkubwa. Aidha, kwa lengo la kutafuta malisho kwa wanyama wawindaji kama vile simba na mamba, tatizo hili huchangiwa pia na ukosefu wa elimu ya uhifadhi wanyamapori kwa vile huwa vigumu kwao kufahamu tabia za wanyama.

Moja ya mikakati inayokabiliana na tatizo la umasikini ni pamoja na mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini, MKUKUTA. Uanzishwa kwa vyama vya msingi vya kuweka na kukopa, SACCOS, kumeleta matumaini makubwa katika kukuza kipato cha mwananchi mmoja mmoja. Hata hivyo, bado wananchi wachache wanaifahamu elimu hii inayounga mkono jitihada za MKUKUTA hususan jamii ya wavuvi na wananchi wengine wanaoishi vijijini.

Ili kuhakikisha kwamba jamii hiyo inakwenda pamoja na mikakati ya serikali ya kupunguza kasi au kuondoa kabisa umaskini, basi hakuna budi elimu ya biashara ielekezwe zaidi vijijini ambako suala la uendeshaji wa biashara ndogo ndogo kwa vikundi bado halijapata nafasi kubwa. Mkakati huu uende sambamba na ongezeko la mtaji kwa vikundi husika. Kwa kufanya hivyo hakutapunguza tu hasara katika kuendesha biashara bali pia kutasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira kunakofanywa na wananchi hususan wavuvi ambao hukata miti kwa ajili ya kukaushia samaki huku vyanzo vya maji vikiharibiwa bila kikomo.



# Jumuiya ya Hifadh
# ya Uyumbu



Kakakuona Oktoba - Desemba 2006

# i Wanyamapori yatia fora

# Karibu Hifadhi ya RU

Tabu Ndziku

**HIFADHI** ya Taifa ya Ruaha, RUNAPA, ni miongoni mwa Hifadhi 14 za Taifa ambazo zimesheheni wanyama wa kila aina, spishi mbalimbali za ndege, wadudu pamoja na mimea ya kila sampuli. Hifadhi hii, ikiwa ni ya pili kwa ukubwa, ndiyo inayoongoza kwa kuwa na Tembo wengi kuliko hifadhi zote. Si hivyo tu, bali hata Tembo wake ni wakubwa ukilinganisha na wale wa hifadhi nyingine kama ile ya Mikumi.

Hifadhi ya Taifa ya Ruaha yenye ukubwa wa kilometa za mraba 10,300 inaweza kuwa ndiyo kubwa kuliko zote kwa kuipiku Serengeti kama wazo la kuunganisha na Pori la Usangu litaendelea kama inavyofikiriwa sasa. Hivi sasa Hifadhi ya Serengeti ndiyo inayoongoza kwa ukubwa kati ya Hifadhi 14 zilizopo nchini. Hifadhi ya Ruaha ilianzishwa mwaka 1964.

Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambayo inajulikana kwa kifupi cha RUNAPA inajiandaa kupokea Pori la Akiba la Usangu kwa kuandaa bajeti itakayoweza kutosheleza kuendesha eneo hilo ikiwa ni pamoja na wafanyakazi na pia kuangalia maeneo mbalimbali ya Pori hilo yatakayovutia watu kwa utalii. Ni wazi kwamba Tindiga la Ihefu ni miongoni mwa vivutio husika.

Hifadhi hii ya Ruaha inapakana na Pori la Akiba la Rungwa-Kizigo-Muhesi kwa upande wa Kaskazini na kwa upande wa Kusini inapakana na Pori la Akiba la Usangu, na Lunda - Mkwambi kwa upande wa Kaskazini Mashariki. Hifadhi hiyo iko umbali wa Kilomtia 138 kutoka Iringa Mjini.

Hifadhi hii ilipewa jina la Ruaha kwa sababu Mto Ruaha Mkuu unapita katikati ya Hifadhi hiyo. Wanyama wa Hifadhi hiyo tegemeo lao kubwa la maji ni kutoka mto huu ambao una manufaa mengi kwa watanzania.

Hifadhi ya Ruaha ina wanyama wa aina nyingi hususan wanyama ambao wanaopatikana katika Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika yaani Sudan, Ethiopia pamoja na ukanda wa Kusini wa Bara la Afrika.

Uwapo Hifadhi ya Ruaha huwezi ukawakosa wanyama kama Kudu wakubwa na wadogo kwa sababu Hifadhi ya Ruaha ndiyo nyumbani kwao. Aidha wanyama kama vile mamba, viboko hupatikana ingawa upungufu wa maji katika miaka ya karibuni na hasa wakati wa kiangazi umewaathiri sana wanyama hao.

Wanyama wengine ni twiga, tembo, simba, duma, mbwa mwitu, kobe, swala, mbweha, chui na wengine wengi huwezi kuwakosa katika hifadhi hiyo.

Hifadhi ya Ruaha inaongoza kwa kuwa na Tembo wengi katika Hifadhi za Taifa. Hifadhi ina Tembo zaidi ya 10,000. Si hivyo tu, hifadhi hiyo pia ina mimea kama "*acacia commoniphora*", pamoja na miombo ambayo zinazopatikana kwa wingi.



# aha kwa utalii

Kutokana na uzuri wa mandhari, utulivu wa eneo na wanyama umeanza kuwavutia watalii wengi hasa wanaopenda utulivu. Karibu kila kitu kilichoumbwa na Mwenyezi Mungu katika hifadhi hiyo bado kingaliko kama zamani. Hakuna uharibifu wa mazingira katika hifadhi hii. "Hifadhi bado ni ardhi bikira."

Kutokana na uzuri huo idadi ya watalii wa ndani na nje umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Kwa mfano, mwaka 1996 kulikuwa na watalii wa nje 2,223 na watalii wa ndani (wazalendo) 1,745. Hata hivyo idadi hiyo imepanda hadi kufikia watalii wageni 11,561 wakati ambapo watalii wa ndani wameongezeka hadi kufikia 4,049.

Ni jambo lisilo kificho kwamba ingawa idadi hiyo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, lakini bado azma ya Tanzania ni kuona idadi inaongezeka zaidi ili hata pato letu liongezeke.


Kwa upande wa watalii wa ndani, yaani wazalendo, ni wakati wa kuwa na mabadiliko katika maisha. Si jambo jema mzungu kutoka nje anakuambia nimetembelea pori au hifadhi fulani na kuona mnyama kama nyati au simba, lakini wewe mwenyewe hujawahi kutembelea wala kumwona mnyama huyo. Viingilio kwa wazalendo ni vidogo mno. Ukiacha kunywa bia mbili au tatu, utakuwa na uwezo wa kutembelea hifadhi.

Hifadhi ina barabara nzuri za kupita na si hivyo tu, hata ukitoka Iringa mjini, barabara ya kwenda huko, japo siyo ya lami, lakini ni nzuri na inapitika wakati wote.

Aidha kuna daraja zuri linalounganisha upande mmoja wa hifadhi na mwingine uliotenganishwa na mto Ruaha Mkuu. Kuanzia mwaka 1990 Daraja la Ibuguziwa lilijengwa na hivyo kutoa nafasi ya magari kupita kwenda upande wa pili wa hifadhi. Ujenzi huo umechangia pia kuongezeka kwa watalii.

Ili kufanikisha shughuli za uhifadhi, uongozi umeishirikisha kikamilifu jamii ya Watanzania wanaoishi kuizunguka hifadhi ili kukabiliana na majangili na watu wasio na mapenzi mema ya uhifadhi. Hii imesaidia kwa kiwango kikubwa kudhibiti ujangili katika Hifadhi ya Ruaha.

Hifadhi hutoa elimu ya uhifadhi endelevu katika vijiji jirani na pia inashiriki katika miradi ya maendeleo na imechangia zaidi ya shilingi 135 milioni katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha yaani 2003/2004, 2004/2005 na 2005/2006.



# Maeneo yaliyohifadhiwa TANZANIA

***Tanzania imetenga karibu robo ya eneo lake kwa ajili ya uhifadhi. Maeneo yaliyohifadhiwa ni pamoja na Hifadhi za Taifa (National Parks), Hifadhi ya Ngorongoro (Ngorongoro Conservation Area) na Mapori ya Akiba (Game Reserves)***

**Hifadhi za Taifa**

**SERENGETI**

**Mbuga Zisizo Mwisho za Majaabu ya Asilia.**

Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, yenye eneo la kilometa za mraba 14763 ni moja kati ya hifadhi kubwa za wanyamapori duniani. Moja kati ya matukio ya kushangaza katika falme za wanyama, ni kuhama kwa maelfu ya nyumbu kunakotokea katika hifadhi hii kila mwaka. Hifadhii ya Serengeti ilikubaliwa na Mkataba wa Urithi wa Dunia kama 'Eneo la Urithi wa Dunia' na kama 'Biosphere Reserve'.

Jina la hifadhi hii, yaani Serengeti, linatokana na neno la Kimasaai- siringet ambalo linamaanisha 'tambarare zisizo na mwisho'. Hifadhi ilitangazwa mwaka 1951 na ipo umbali wa kilometa 320 kutoka mjini Arusha.

Sura ya nchi ya Hifadhi inatofautiana kuanzia eneo kubwa lisilo na miti la katikati ya mbuga ya Serengeti na sehemu ndefu za savanna zenye mti mmoja mmoja aina ya migunga, mawe ya kupendeza yanayojitokeza yaitwayo 'kopjes', vichaka vya kandokando ya mito, vichaka vinene kwenye vijito, mito, kinamasi ndogo na maziwa. Maumbile haya huipatia hifadhi hali nyingi na tofauti za kuvutia.

Hifadhi inayo wanyamapori wakubwa wapatao milioni tatu, wengi wao wakiwa wanashiriki katika kuhama mara msimu unapowadia, moja kati ya maajabu ya asilia. Kuhama kila mwaka kwa zaidi ya nyumbu milioni 1.5 pamoja na maelfu ya pundamilia na swala kunasabishwa na mvua.

Hifadhi ya Serengeti inayo spishi 35 za wanyama waishio mbugani, kuanzia sungura hadi tembo na aina ya ndege wazuri. Makadirio ya savei ya idadi ya wanyama inaonyesha kuwepo wanyama wapatao milioni nne wakijumuisha simba 3000, nyumbu 1,6000,000 na pundamilia 500,000. Zipo spishi zaidi ya 400 za ndege.

**Huduma kwa wageni:** Zipo hoteli nne, kambi za mahema sita na maeneo ya kuweka kambi ya muda za aina tofauti.

**TARANGIRE:**

**Chatu Wanaopanda Miti**

Tarangire, inayokadiriwa kuwa na kilometa za mraba 2600, ipo kusini mwa eneo kubwa la mbuga za tambarare kusini kabisa mwa mbuga ya Maasai, kilometa 115 kutoka Arusha katika barabara ya Arusha kwenda Dodoma.

Mazingira ya Hifadhi ya Tarangire ambayo yanarandana na aina ya wanyama wanaopatikana katika eneo hili zipo mbuga na tambarare zinazosimama maji. Tarangire ni maarufu kwa chatu wanaopanda miti, kongoni, tembo, nyati, kuro, swala, choroa na ndege wa aina nyingi.

**Huduma kwa wageni:** Hoteli, kambi za mahema na maeneo ya kuweka kambi ya muda vinapatikana ndani ya hifadhi.




**ZIWA MANYARA:**

**Simba kwenye matawi ya migunga**

Umbali wa kilometa 125 magharibi mwa mji wa Arusha, chini ya ukuta wa Bonde la Ufa, Hifadhi ya Ziwa Manyara ilipata hadhi yake mwaka1960. Hifadhi hii ina ukumbwa wa kilometa za mraba 330, ambapo kati ya hizo 230 ni Ziwa Manyara.

Hifadhi inayo makazi makubwa ya aina nyingi kama vile ukuta wa Bonde la Ufa, msitu wa asili ya maji ndani ya ardhi, mapori ya migunga, maeneo ya wazi ya mbuga, kwa uchache tu, hivyo kufanya Hifadhi hii

# RAMANI YA TANZANIA




(Baadhi ya Mapori ya Akiba yaliyoanzishwa hivi karibuni hayapo katika Ramani hii).

kuwa na uwezo wa kuwa na spishi nyingi za wanyama.

Mnyama wa kuvutia kuliko wote katika hifadhi ni simba wapandao miti, ambao mara nyingine huonekana katika matawi ya migunga.

Wanyama wengine wanaopatikana katika eneo hili ni pamoja na tembo, chui, swala, viboko na mamilioni ya ndege maji (korongo). Ziwa linavutia ndege wengi kuwepo katika hifadhi hii.

Hifadhi ya Ziwa Manyara inayo idadi kubwa ya tembo wa Tanzania katika kila kilometa moja.

**Huduma kwa Wageni:** Kambi za muda, kambi za mahema na hoteli. Nyumba za kulala wageni zinapatikana karibu na eneo la hifadhi na zinatoa huduma nzuri ya malazi na chakula.

### ARUSHA

### Mahali unapoweza kuangalia ndege katikati ya Vilele vya Milima mirefu

Hapo zamani ikijulikana kama Hifadhi ya Taifa ya Ngurdoto Crater hadi mwaka 1967. Hifadhi ya Taifa ya Arusha ina ukubwa wa kilometa za mraba 137. Hifadhi hii ipo karibu kabisa na mji wa Arusha katikati ya vilele vya Mlima Kilimanjaro na Mlima Meru. Jina hili la hifadhi na mji linatokana na watu wa asili wa walioishi katika eneo hili wajulikanao kama Waarusha.

Ngurdoto crater, Maziwa ya Momela, misitu ya uwanda wa juu, na Mlima Meru - mita 4,575 kutoka usawa wa bahari - ni alama pekee nne k[illegible] nyani, funo mwekundu, mbega, tumbili, nyati, viboko, pongo, na twiga. Ndege, na hasa ndege maji ni wengi na wa kufurahisha.

**Huduma kwa wageni:** Hoteli ya Momela ndani ya hifadhi inatoa malazi na chakula kizuri. Sehemu nyingine za kukaa ni nyumba ya wageni ya hifadhi na sehemu za kipekee za kuweka kambi.



### KILIMANJARO:

### Mlima Mrefu kuliko yote Afrika



Katika eneo la kilometa za mraba 756, Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ilipata hadhi yake mwaka 1973. Hifadhi hii ipo kwa ajili ya kulinda mandhari nzuri kabisa na wanyama na mimea ya Mlima Kilimanjaro Ukiwa meta 5,895 kutoka usawa wa bahari, Mlima Kilimanjaro ni mrefu kuliko yote Afrika, mlima uliosimama peke yake mrefu kuliko yote ulimwenguni na moja ya volkano kubwa ambazo zimeshawahi kutokea katika ardhi.

Volkano zake tatu ndiyo sehemu zake kuu za kipekee: Shira kwa upande wa Magharibi (mita 4,269), Mawenzi kwa upande wa Mashariki (mita 5,280) na katikati Kibo iliyofunikwa na theluji (mita 5,895), kati ya volkano za hivi karibuni na iliyosinzia.

Zaidi ya vilele na ardhi yenye vichaka vilivyodumaa, msitu wa mlimani na mabaki ya mimea ya kale hupatikana katika hifadhi hii. Idadi nzuri ya wanyama wa kundi la mamalia, ndege na wadudu pia wanaishi humo.

Wanyama kundi la mamalia ni pamoja na tembo, nyati, pofu, mindi, chui, nyani, kima, na mbega. Ndege mbalimbali pia hupendelea kutembelea hifadhi hii.

Kupanda na kushuka mlima huchukua muda wa siku tano hadi sita. Mtu yeyote mwenye afya nzuri anaweza kupanda mlima kwa kusaidiwa na muongozaji na mbeba mizigo. Hifadhi inazo sehemu sita za kupandia mlima, kupitia Msitu wa Hifadhi wa Kilimanjaro-Marangu, Mweka, Umbwe, Machame, Shira na Rongai.

Makao makuu ya hifadhi yapo Marangu pembeni kabisa mwa msitu na yanafikika kwa kutumia njia ya

lami umbali wa kilometa 48 kutoka Moshi na kiasi cha kilometa 90 kutoka uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro.

**Huduma za wageni:** Hoteli na loji zipo karibu na hifadhi na mjini Moshi.

### MIKUMI

**Karibu na Dar es Ssalaam**

Pembezoni mwa barabara kuu itokayo Dar es Salaam kwenda Zambia ndipo ilipo Hifadhi ya Taifa ya Mikumi yenye eneo la kilometa za mraba 3,230 na ya tatu kwa ukubwa katika Tanzania.

Hifadhi hii inafikika kwa urahisi kuliko hifadhi zote, kwa kutumia barabara au ndege ndogo za kukodisha.

Hifadhi ya Mikumi ipo katikati ya milima iliyoinuka na miinuko yenye misitu ya Mto Mkata. Kwa upande wa Mashariki zipo safu za milima ya Uluguru inayoinukia kufikia futi 900, wakati upande wa Kusini-Magharibi vipo vilele vinavyochomoza vya milima ya Lumango.

Hifadhi hii inao wanyamapori wengi na wanyama kama nyati, simba, nyumbu, pundamilia, swala, ngiri na tembo wanaweza kuonekana kirahisi wakati wote wa mwaka. Reptilia wanaoishi katika hifadhi hii ni pamoja na mamba, kenge na chatu.

Spishi za ndege zipatazo 300 zimeshawahi kuainishwa kimaandishi, baadhi yake zikiwa ni wa maji kutoka Bara la Ulaya na Asia.

**Huduma kwa Wageni:** Hoteli ya Mikumi na Kambi ya Mikumi na Vuma zinatoa malazi na chakula kizuri. Vilevile yapo maeneo ya kuweka kambi za muda na hosteli ya vijana.

### GOMBE

**Maarufu kwa Wanyama aina ya 'primata'**

Ikiwa katika eneo la kilometa za mraba 52 kiasi cha kilometa 16 Kaskazini mwa mji wa Kigoma Magharibi ya Tanzania, Gombe ni eneo jembamba la ardhi ya milima inayokingwa na kingo za juu za ukuta wa Bonde la Ufa upande wa mashariki na Ziwa Tanganyika kwa upande wa magharibi.

Uzuri wa Hifadhi ya Taifa ya Gombe ni wa kipekee; ni hifadhi isiyo na barabara, ambapo unaweza kutembea na kupata hisia zote za mazingira asilia.

Kutokana na umbali toka usawa wa bahari, mimea iliyopo hifadhini inatofautiana kuanzia misitu ya kijani kibichi yenye miti mirefu hadi nyika na mbuga. Mamalia wanaopatikana kila wakati katika hifadhi ni spishi za misituni hususan primata. Hawa ni pamoja na sokwemtu, kima, kima wenye mkia mwekundu na mbega mwekundu.

Kwa kweli hifadhi hii ni kisiwa cha mazingira asilia ya kipekee kilichozungukwa na mashamba katika pande tatu na ziwa kwa upande wa kaskazini.

**Huduma kwa wageni:** Ipo hosteli na sehemu za kambi za muda, na hoteli katika mji wa Kigoma.

### MILIMA YA MAHALE

**Sokwemtu katika makazi ya asilia**

Hifadi ya Milima ya Mahale ipo kilometa 120 kusini mwa mji wa Kigoma kwenye sehemu ya ardhi ya nchi kavu inayochomoza na kuingia ndani ya Ziwa Tanganyika. Hifadhi hii imetawaliwa na safu ya Milima ya Mahale kutokea kaskazini magharibi hadi katikati ya hifadhi. Kilele kirefu kabisa kipo mita 2,462 kutoka usawa wa bahari.

Mimea imetawaliwa na miti ya miombo na safu nyembamba za misitu inayoambaa na mito. Hifadhi hii inayo makazi yenye wanyama wa aina nyingi kuanzia tembo, ngiri, twiga, pundamilia, korongo, nyati, fisi, mbwa mwitu hadi simba kwenye nyika ya mashariki. Sokwemtu na kima wanapatikana pia Mahale. Kulingana na taarifa za utafiti wapo sokwemtu 700 katika makundi yapatayo 15.

**Huduma kwa wageni:** Karibu na kijiji cha Kasiha ipo nyumba ndogo ya kulala wageni na kambi ya muda ya kifahari ambayo huwa inafunguliwa msimu wa kiangazi tu (May-Oktoba).

### KATAVI

**Mazingira Asilia katika hali ya Asili**

Hifadhi ya Taifa ya Katavi ipo katika Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Rukwa kiasi cha kilometa 40 kusini mashariki mwa mji wa Mpanda.

Hifadhi hii inasifika kwa kuwa na sura asilia ambayo haijaguswa ukilinganisha na hifadhi nyingine nchini. Mimea inayopatikana kwa wingi ni nyika ya miti ya miombo pamoja na migunga ya hapa na pale karibu na Ziwa Chada. Ziwa Chada linao utajiri mkubwa wa ndege na idadi kubwa ya mamba nchini.

Vivutio vikuu ni pamoja na Ziwa Katavi na majani mafupi katika tambarare ya mafuriko kwa kaskazini, Ziwa Chada lilizungukwa na mitende upande wa kusini mashariki na Mto Katuma. Wanyama wanaopatikana katika hifadhi hii ni pamoja na pundamilia, palahala, korongo, pofu, tembo, nyati, simba, chui na ndege-maji.

**Huduma kwa Wageni:** Nyumba ya kupumzikia na maeneo ya kuweka kambi yapo ndani ya hifadhi, na hoteli na loji zipo mjini Mpanda na Sumbawanga.

**RUBONDO**

**Inaelea katika Ziwa kubwa kuliko yote Afrika**

Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo ipo magharibi mwa mji wa Mwanza. Ni ya kipekee kutokana na ukweli kuwa ndiyo hifadhi pekee katika Ziwa Victoria.

Ziwa Victoria ndilo kubwa katika Afrika na la pili kwa ukubwa katika dunia; ikiwa linalifuatia Ziwa Superior. Hifadhi inayo makazi ya aina nyingi kuanzia mapululu ya savanna hadi nyika za wazi, misitu minene na vinamasi vya matete. Spishi za wanyama wapatikanao ndani ya hifadhi ni pamoja na viboko, mamba, pongo, nzohe, twiga, tembo na sokwemtu.

Hifadhi ya Rubondo ni ya kipekee pia kwa upande wa ndege. Ndege kutoka mashariki, katikati na kusini mwa Afrika wanaweza kuonekana wakizaliana katika 'kisiwa cha ndege'.

**Huduma kwa Wageni:** Yapo maeneo ya kuweka kambi za muda na ya po mabanda ya kulala wageni.

**UDZUNGWA**

**Hazina kubwa ya Spishi Adimu**

Hifadhi hii ni mpya kuliko zote nchini, na ipo katika mikoa ya Morogoro na Iringa upande wa Kusini-Kati ya Tanzania. Imepakana na Mto Ruaha Kubwa kwa kaskazini na barabara ya Mikumi-Ifakara kwa upande wa mashariki. Hifadhi ya Milima ya Udzugwa ina ukubwa wa kilometa za mraba 1900. Makao makuu yake yapo Mang'ula, kiasi cha kilometa 60 kutoka Mikumi.

Kivutio kikuu cha hifadhi hii ni misitu anuwai kibaiolojia na upekee wake. Vilevile, Hifadhi ya Milima ya Udzungwa inayo spishi za mimea ambazo hazipatikani sehemu yoyote duniani kuanzia mmea mdogo kabisa uitwao 'African violet' hadi miti yenye urefu wa mita thelathini.

Zaidi ya hifadhi kuwa na spishi sita za primata, nyanda zake zinao wanyama kama tembo, nyati, simba, chui, mbwa mwitu na spishi nyingi za ndege wa msituni *ikiwa ni pamoja na 'Modulatrics O. Sanjel' aina ya kwale wanaopatikana katika hifadhi hii tu waliogunduliwa mwaka 1979.*

**Huduma kwa Wageni:** Chakula kizuri na malazi yanapatikana Twiga Risoti karibu kabisa na lango la kuingilia hifadhini. Kwa wale wenye vifaa vya kuweka kambi, yapo maeneo matatu yaliyotengenezwa ndani ya hifadhi kwa ajili hiyo. Katika kijiji cha Mang'ula yanapatikana mahitaji ya lazima na soko.

**RUAHA**

**Ndoto ya Watalii Afrika**

Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ni ya pili kwa ukubwa katika Tanzania ina eneo la kilometa za mraba 12,950. Kwa wale wanaopenda kwenda sehemu ambayo hawataona watu wengi au kuona simba akiwa na mnyama wake aliyemkamata akiwa hajazungukwa na magari , hii ndiyo sehemu yake. Hifadhi ya Ruaha ni Afrika ambayo watu wengi wanaota ndoto.

Wakati mzuri zaidi wa kutembelea hifadhi ni katika msimu wa kiangazi kati ya mwezi Mei hadi Novemba, kutokana na kutopitika kwa sehemu kubwa ya barabara ziendazo hifadhini wakati wa masika.

**Huduma kwa Wageni:** Loji ya Ruaha iliyojengwa kwenye mawe na inayoangalia Mto Ruaha inatoa malazi na chakula kizuri. Sehemu nyingine ya malazi ni kwenye kambi za mahema sehemu mbalimbali katika hifadhi, mabanda, hosteli na maeneo ya kuweka kambi.

**ENEO LA HIFADHI LA NGORONGORO**


**Mahali Alipoanzia Binadamu**

Eneo la Hifadhi la Ngorongoro ni eneo kubwa len volkano hai, milima, maeneo ya mambo ya ka tambarare zinazojiviringa, misitu, maziwa, vilima mchanga na Kreta ya Ngorongoro na Olduvai Gor

Katika Afrika, Ngorongoro ndiyo yenye wanya wanaokula nyama wengi zaidi kwa eneo. Wap wanyama wakubwa wapatao 25,000, ambao zaidi ni swala, nyati, pofu, kongoni na ngiri. Vifaru weusi pia wanapatikana Ngorongoro.

**Huduma kwa Wageni:** Zipo hoteli za hadhi ya nyota tano mbili zinaoangalia kreta na loji moja. Pia yapo maeneo ya kuweka kambi za muda.

**MAPORI YA AKIBA**



**Kuna mapori ya akiba yafuatayo:**

- Selous
- Moyowosi/Kigosi
- Burigi/Biharamulo
- Rungwa/Kizigo
- Maswa
- Ibanda/ Rumanyika
- Saanane Island
- Mkomazi
- Ugalla
- Lukwikwa/Lumesule
- Pande
- Ikorongo/Guruneti
- Swagaswaga/Mkurunero
- Rukwa
- Usangu
- Mpanga/Kipengele

### PORI LA AKIBA LA SELOUS

### Se[illegible] asilia ya Dunia ambayo Haijaharibiwa

Li[illegible] jina lake kutokana na mwindaji na m[illegible]mu wa mazingira asilia Frederick Courtney Sel[illegible] aliyefariki mwaka 1917. Selous alizikwa katika pori hili na kaburi lake linaweza kuonekana kwa ku[illegible] barabara ya Beho Beho-Matambwe. Pori la Akiba la Selous ni eneo lililohifadhiwa kisheria, kubwa kuliko yote duniani, linalofikia kilometa za mraba 50,000. Ni kubwa kuliko eneo la nchi ya Switzerland au Denmark. Hakuna mtu anayeishi huko na hakuna shughuli nyingi za binadamu huko. Kutokana na upekee wa ikolojia yake muhimu pori hili lilitangazwa na Umoja wa Mataifa kuwa Eneo la Urithi wa Dunia mwaka 1982.

Pengine ndilo pori pekee lenye mazingira asilia kabisa lililobakia katika Afrika. Kuna shughuli za maendeleo kidogo sana zinazofanyika hapa. Siyo zaidi ya watalii 4,000 wanatembelea pori hili kwa mwaka, na hii ndiyo hali inaoongeza raha ya kutembelea pori hili. Kwa makusudi huu ndiyo utalii uanoendelezwa na mamlaka ya Pori hili, ili kufanya eneo hili kuwa tofauti na hifadi na mapori mengine ya Afrika.

Katika pori hili unaweza kuendesha safari za boti katika mito. Hakuna eneo jingine Tanzania ambalo unaweza kufanya hivi, kuangalia wanyama hasa kandokando ya mito na maziwa. Pia unaweza kutembea kwa miguu, kitu ambacho hakifanywi katika hifadhi na mapori mengi.

Pori la Selous lipo umbali wa kilometa 250 kutoka Dar es Salaam kupitia njia ya Kibiti, Mkongo na Mloka hadi lango la Mtemere, au kilometa 350 kutoka Dar es Salaam hadi lango la Matambwe kupitia Morogoro na Matombo. Unaweza pia kwenda Selous kwa njia ya ndege ndogo za kukodi na unaweza kutua katika viwanja vya Mtemere, Mbuyu, Beho Beho, Sand Rivers, Stieglers Gorge na Kambi ya Selous Safari. Reli ya TAZARA inapita eneo la kaskazini mwa pori hili. Inachukua muda wa masaa manne kutoka Dar es Salaam hadi stesheni ya Fuga au stesheni ndogo ya Matambwe ambapo utashuka.

Pori la Akiba la Selous na maeneo yanayolizunguka yanakaliwa na tembo wapatao 60,000. Wanyama wengine ni pamoja na nyati 160,000, viboko 40,000, simba 5,000, mamba na wanyama jamii ya swala wengi, japo ni tembo aliyefanya pori hili liwe na sifa kemkem. Wapo ndege wapatao spishi 440. Kutokana na ukubwa wake, umbo la nchi, mito na maziwa Selous inayo makazi anuwai ya wanyama, ikiwa ni pamoja na mapululu ya wazi, nyika za migunga na miombo na misitu inayoambaa na mito. Vinamasi ni makazi muhimu kwa mimea ya ardhioevu, reptilia na ndege wahamiaji na wale wenyeji. Zaidi ya Mto Rufiji, Ziwa Tagalala na maporomoko ya Stieglers ni moja ya vivutio vikuu vya Selous.

**Huduma kwa Wageni:** Kuna kambi za watalii za kifahari sita zinazotoa malazi na chakula kizuri. Yapo maeneo mawili ya kudumu kwa ajili ya kuweka kambi, na maeneo maalum ya kuweka kambi ambayo nafasi yaweza kupatikana kwa kupeleka maombi ya nafasi kwa uongozi wa pori kabla ya kufika huko.

UNIVERSITY OF AGR... LIBRARY



# Hongera Nalika kwa Uhifadhi wa Wanyamapori

Na Ruha Josephat

**NALIKA** ni Jumuiya ya Jamii ya Hifadhi ya Wanyamapori iliyoko Kusini mwa Tanzania katika wilaya ya Tunduru mkoa wa Ruvuma, Kusini mwa Pori la Akiba la Selous. Jumuiya hii imeundwa na vijiji kumi vya kata za Namwinyu, Ligunga na Kalulu. Jina NALIKA linatokana na vifulisho vya Kata hizi tatu. Vijiji vilivyounda Jumuiya hiyo ni Rahaleo, Mbungulaji Kindamba, Kajima, Twendembele, Namwinyu, Namakungwa, Ndenyende, Hulia na Darajambili. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2002, eneo hili lina jumla ya wakazi wapatao 16,000. Jumuiya ilisajiliwa rasmi mwaka 2004 kwa kufuata kanuni na sheria za usajili wa Jumuiya ya ikiwa na Namba ya usajili S0 Na 2702. Jumuiya ya Jamii ya NALIKA inasimamia uhifadhi katika eneo la majaribio la Hifadhi ya Wanyamapori ya Liwale.

Mipaka ya eneo la majaribio la Jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori la Liwale inaanzia kwenye makutano ya mito Muhuwesi na Michonjo kuelekea vilima vya Ngunguru na kuungana na Pori la Akiba la Selous kwa upande wa Kaskazini. Upande wa Magharibi Jumuiya imepakana na chanzo cha mto Lipembe karibu na vilima vya Kilimasera vilivyoko katika wilaya ya Namtumbo na Tunduru. Kwa Upande wa Kusini eneo hilo limepakana na barabara kuu iendayo Songea hadi Tunduru kwenye milima ya Lihowela. Na kwa upande wa Mashariki eneo linapakana na mto Nampungu mpakani mwa vijiji vya Ndenyende, Nampungu na Mbatamila.

Katika eneo la Jumuiya kuna vivutio vingi vya utalii ambavyo kama vitaendelezwa na kutangazwa ndani na nje ya nchi vitaliongezea Taifa kipato.Vivutio hivi ni pamoja na wanyamapori kama tembo wenye meno makubwa na yaliyokomaa yenye uzito mkubwa kwa mujibu wa taarifa za uwindaji mwaka 2000. Wanyama wengine ni pamoja na Simba, Chui, Pofu, Palahala na Nyati ambao wamekuwa vivutio vikubwa kwa watalii wa ndani na nje wanaofika katika eneo la jumuiya kwa ujumla. Mbali na wanyama kuna miti ya asili na ya aina nyingi ambayo hutumika kwa matumizi ya kila siku ya binadamu kama vile ujenzi wa nyumba, kuni, vivuli, miti ya matunda, madawa, n.k.

Pia kuna ushoroba wa Wanyamapori uliopita katikati ya baadhi ya vijiji vinavyounda Jumuiya ambapo makundi makubwa ya wanyampori huonekana wakati wakipita kutoka eneo moja kwenda jingine. Zipo hata chemchem na mito ambayo huhifadhi maji kwa kipindi chote cha mwaka, hivyo kunakuwa na samaki wa aina mbali mbali ambao hutumika kwa kitoweo kwa watu wa NALIKA. Pembeni mwa chemchem na mito hiyo kuna uoto mzuri wa nyasi, na vichaka ambavyo hutumiwa na wanyamapori kama sehemu ya kupumzikia hasa nyakati za jua kali.

Hali ya mazingira na uoto katika eneo hili ni nzuri na ya kuvutia kwani vijiji vyote kumi vinavyounda Jumuiya vinazungukwa na mapori ya Akiba ya Selous na Sasawala. Pia eneo hili ni miongoni mwa maeneo katika wilaya ya Tunduru ambayo hayajaathiriwa sana kimazingira kama vile ufugaji holela, uchomaji moto ovyo n.k.

Pamoja na kuwepo kwa vivutio vyote hivyo bado eneo hili la majaribio halijaweza kukamilisha taratibu zinazotakiwa kulingana na Sheria na Kanuni za maeneo ya Jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori ili kuidhinishwa na kutangazwa kuwa eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori (CBO) na kupata hadhi ya Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa. Hivyo bado tunaendelea kukamilisha taratibu hizo ili eneo



letu, liweze kuwa WMA na Jumuiya kuwa Jumuiya iliyoidhinishwa (AA).

Matukio ya ujangili yamepungua sana katika maeneo ya Hifadhi ikilinganishwa na maeneo ambayo hayapo katika mchakato wa kuanzisha maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori. Hii imetokana na doria zinazofanywa na askari wa vijiji.husika kila mwezi na utaratibu mzuri wa uhifadhi zikiwemo sheria ndogondogo za udhibiti wa ujangili na uhifadhi endelevu wa maliasili katika eneo la Jumuiya.

Pia hii imetokana na wananchi kunufaika na maliasili zinazopatikana ndani ya eneo kama uwindaji wa "quota" ambapo kila mwanajumuiya anaruhusiwa kununua nyama kwa bei nafuu ya Tsh 800/= kwa kilo moja, ambapo kama familia haina hela inaruhusiwa kubadilisha nyama kwa mazao mengine kama vile maharage na mahindi ambavyo hutumika kwa ajili ya chakula cha doria kwa askari wa Vijiji husika. Kutokana na faida wanazozipata wananchi muda mwingi wamekuwa macho katika kulinda eneo la Jumuiya lisiingiliwe na majangili kutoka nje.


**Mafanikio yaliyofikiwa**

Kutokana na ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi wa wanyamapori na mazingira tayari jamii imeshajipatia mafanikio mengi katika maeneo yao. Mfano mzuri wa mafanikio hayo ni ujenzi wa zahanati, ukarabati wa nyumba za walimu, na za wakunga, pamoja na ujenzi wa pampu ya maji. Kutokana na hayo wananchi wamekuwa mstari wa mbele katika kuhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili katika eneo lao. Mafanikio mengne ni kwa jumuiya kupata mgao wa asilimia 25% ya mapato ya uwindaji unaofanywa katika eneo hilo na hivyo mapato hayo kuweza kusaidia katika miradi mingine ya maendeleo kama ile ya kilimo, vikundi vya akina mama na vijana ili kuweza kukabiliana na mchakato mzima wa kutekeleza MKUKUTA. Si hivyo tu bali kumekuwepo na ongezeko kubwa la wanyama wa aina mbalimbali kama vile Tembo, Nyati na wengineo katika eneo la hifadhi, pamoja na kupungua kwa matukio ya ujangili hususan baada ya elimu ya uhamasishaji kutolewa ikilinganishwa na wakati wa nyuma kabla ya kutolewa kwa elimu hiyo.

Tangu kuanzishwa kwa jumuiya na mpango wa ushirikishaji wa Jamii katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili kumekuwa na mabadiliko chanya ya kiuchumi na kijamii miongoni mwa wananchi husika, kwani wengi wamenufaika sana wameridhika na kuukubali mpango huo.

NALIKA sasa inakabiliwa na suala la kukamilisha hatua zilizosalia katika mchakato mzima wa kuanzisha eneo la Jumuia ya Hifadhi ya Wanyamapori na kisha Jumuiya ya Jamii ya NALIKA kupatiwa hadhi ya kuidhinishwa kuwa Jumuiya ya Jamii iliyoidhinishwa.





Graphic Design • Prepress • Full Colour Printing • Hexachrome Printing

TANZANIA PRINTERS

Plot No. 126/2 Mbozi Rd. Chang'ombe,
P.O. Box 451, Dar es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 22 2866776-80, Telefax: +255 22 2866775
Website: www.tanzaniaprinters.com
E-mail: info@tanzaniaprinters.com

# MFUKO WA KUHIFADHI WANYAMAPORI TANZANIA

Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - Tanzania Wildlife Protection Fund (TWPF) ulianzishwa kwa Sheria ya Bunge namba 21 ya mwaka 1978 kufuatia marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori namba 12 ya 1974. Mfuko ulianzishwa kwa madhumuni ya kuziba mapengo ya mahitaji ya uhifadhi.

Kazi muhimu za uhifadhi zinazopatiwa fedha na Mfuko kupitia vikao vya Bodi ya Wadhamini ni:

- Usimamizi na uendelezaji wa Mapori ya Akiba
- Matumizi bora ya wanyamapori na mazingira yao
- Mafunzo na shughuli za utafiti wa wanyamapori na mazingira yao
- Hima sheria, uzuiaji wa ujangili na ulinzi wa wanyamapori
- Elimu ya uhifadhi

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Katibu Tawala,
Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania,
Ivory Room, Barabara ya Nyerere
S.L.P. 1994,
DAR ES SALAAM.

Simu: 255 22 2866377
0713 350405
0784 402927/8